



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

06 MACHI, 2025 - Dodoma

TAARIFA KWA UMMA
KUFUTWA UONGOZI WA KAMISHENI YA NGUMI ZA KULIPWA TANZANIA (TPBRC)

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Prof. Palamagamba Kabudi ameufuta Uongozi wa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC) baada ya uchunguzi na tuhuma mbalimbali zilizowasilishwa na wadau wa mchezo wa ngumi.

Ili kuhakikisha uwazi na haki, Mnamo tarehe 8, Mei 2024, Waziri aliunda Kamati Maalum ya Uchunguzi yenye jukumu la kuchunguza malalamiko hayo na kubaini ukweli wake.

Baada ya kamati kukamilisha uchunguzi iliwasilisha taarifa ya yaliyobainika kulingana na tuhuma zilizowasilishwa. Kamati imejidhihirisha pasi na shaka kuwa uongozi ulikuwa na mapungufu ya kiutendaji ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

- (i) Matumizi mabaya ya madaraka kinyume na Sheria za nchi, Katiba ya Kamisheni ya ngumi za kulipwa Tanzania ya mwaka 2018 pamoja na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na usimamizi wa rasilimali za kamisheni.
- (ii) Matumizi mabaya ya fedha kinyume na Sheria za nchi, Katiba ya Kamisheni ya bNgumi za kulipwa Tanzania 2018 pamoja na kanuni za uwajibikaji na usimamizi wa rasilimali za kamisheni.

Kufuatia mapungufu hayo, Mheshimiwa Waziri ameelekeza hatua zaidi za kisheria zichukuliwe dhidi ya viongozi walioondolewa madarakani, ili kuweka fundisho kwa viongozi wengine wa vyama na mashirikisho na michezo nchini.

Hivyo, taarifa hii iwafikie pia viongozi wa vyama na mashirikisho mengine ya michezo nchini kuwa, wazingatie utawala bora unaofuata misingi ya katiba kulingana na taasisi zao na katika nyadhifa wanazoshikilia katika taasisi hizo. Serikali ipo macho na itaendelea kutetea maslahi na mienendo bora itakayochochea ustawi wa michezo wanayoismamia.

Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO